JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA DARASA LA PILI STADI YA KUSOMA NA KUHESABU
KWA KUTUMIA TABLET (KISHIKWAMBI)

## SEHEMU A

201 STADI YA KUSOMA

1. Kusoma kifungu cha maneno kwa ufasaha, umakini na kasi inayotakiwa. (alama 25).

**Maelekezo kwa Msimamizi**

Gusa kila neno ambalo mwanafunzi atashindwa kulisoma na neno hilo litakuwa na rangi **nyekundu**. Iwapo uligusa neno ambalo mwanafunzi alikosea kusoma na akarudia kusoma kwa usahihi, **gusa tena** neno hilo na rangi nyekundu itaondoka.

(a) Mwelekeze mwanafunzi kusoma kifungu cha maneno kwa sauti, umakini na haraka kadri awezavyo. Mwanafunzi atakapokuwa anasoma, fuatilia usomaji wake kwa kutumia kifungu cha maneno kilichopo katika **tablet**.

(b) Iwapo mwanafunzi atashindwa kusoma neno baada ya **sekunde 3**, mwelekeze kusoma neno linalofuata.

(c) Iwapo mwanafunzi atashindwa kusoma **maneno yote** ya sentensi ya kwanza kishikwambi kitasitisha zoezi hivyo endelea na stadi ya kuhesabu.

(d) Iwapo mwanafunzi atasema **sijui** wakati akisoma neno, chukulia kama ni **kosa**.

(e) Iwapo mwanafunzi atashindwa kumaliza kusoma kifungu cha maneno ndani ya **sekunde 60, gusa (hold)** kwa muda neno la mwisho alilosoma mwanafunzi.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

**Maelekezo ya Msimamizi kwa Mwanafunzi**

Karibu ..........Hujambo?

(a) Hapa kuna kifungu cha maneno, nikisema anza utasoma (mwoneshe mwanafunzi kwa kugusa kwa kalamu) kuanzia neno la kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari.

(b) Utasoma maneno kwa sauti, umakini na kwa haraka kadri uwezavyo.

(c) Weka kidole kwenye neno la kwanza. Je uko tayari? Anza.

2. Kusoma kifungu cha maneno kisha kujibu maswali kwa mdomo (alama 25).

**Maelekezo kwa Msimamizi**

(a) Mwongoze mwanafunzi kusoma tena kifungu cha maneno (mwoneshe kwa kugusa kwa kalamu kuanzia sentensi ya kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari). Baada ya mwanafunzi kusoma ndani ya **dakika 3**, chukua karatasi ya mwanafunzi kisha muulize maswali yaliyopo kwenye tablet.

(b) Mwanafunzi akitoa jibu sahihi gusa alama ya **vema** (√), iwapo atatoa jibu lisilo sahihi gusa alama ya **kosa** (X). Endapo mwanafunzi atatoa jibu lisilo sahihi na kisha kufanya marekebisho kwa kutoa jibu sahihi gusa alama ya **vema** (√).

(c) Iwapo mwanafunzi ataulizwa swali na kushindwa kujibu ndani ya **sekunde 10**, utatakiwa kugusa alama ya **kosa** (X) kisha kuendelea na swali linalofuata.





Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

**Maelekezo ya Msimamizi kwa Mwanafunzi**

(a) Utasoma tena kifungu cha maneno (mwoneshe mwanafunzi kwa kugusa kwa kalamu kuanzia sentensi ya kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari).

(b) Utasoma maneno kwa sauti, umakini na kwa haraka kadri uwezavyo. Baada ya kusoma nitachukua karatasi yako kisha nitakuuliza maswali yanayotokana na kifungu cha maneno ulichosoma. Je upo tayari? Anza.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU B

## 203 STADI YA KUHESABU

**Maelekezo kwa Msimamizi**

Gusa alama ya **vema** (√) kwenye **tablet** endapo mwanafunzi atajibu kwa usahihi swali husika au alama ya **kosa** (X) iwapo mwanafunzi atatoa jibu lisilo sahihi. Iwapo mwanafunzi atatoa jibu lisilo sahihi na kisha kufanya marekebisho kwa kutoa jibu sahihi gusa alama ya **vema** (√).

(a) Mwongoze mwanafunzi kujibu maswali ya kujumlisha na kutoa. Mpe karatasi na penseli kisha mwambie kuwa anaweza kutumia kama anataka lakini sio lazima.

(b) Iwapo mwanafunzi atatumia njia isiyoridhisha muulize kama anaweza kutumia njia nyingine.

(c) Iwapo mwanafunzi ataendelea kutumia njia isiyoridhisha au atasimama/atakwama/hatajibu kwa **sekunde 5** kisha endelea na swali linalofuata.

(d) Sitisha zoezi endapo mwanafunzi atakosa maswali **manne** ya mwanzo katika maswali ya kujumlisha kisha endelea na maswali ya kutoa.

(e) Iwapo mwanafunzi atakosa maswali **manne ya mwanzo** katika maswali ya kutoa sitisha zoezi. Endelea na mwanafunzi anayefuata.





Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

**Maelekezo ya Msimamizi kwa Mwanafunzi**

(a) Hapo kuna maswali ya kujumlisha na kutoa (mwoneshe mwanafunzi kwa mkono swali la 1 hadi la 5 kisha swali la 6 hadi 10).

(b) Utaanza na swali la 1. Utajibu maswali hayo kwa mdomo. Unaweza kutumia penseli na karatasi kama unataka lakini sio lazima. Je upo tayari? Anza.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org